



Siku za
16 Uanaharakati
2025
Dhidi ya Ukatili wa Kijinsia

Kauli Mbiu: Fikiria Upya Mustakabali wa Kifeministi: Kuimarisha Mshikamano, kustawi baada ya Migogoro.

Mwongozo wa Shughuli za Vyombo vya Habari

Utangulizi:

Mwongozo huu wa shughuli za vyombo vya habari unatoa zana za kutendea kazi ili kusaidia Kampeni ya Siku 16 za Uanaharakati za Kupinga Ukatili wa Kijinsia. Katika dunia ya leo, migogoro inayoingiliana; kama vile vita, umaskini, mabadiliko ya hali ya hewa, na kuongezeka kwa matumizi mabaya ya mtandaoni, kunaongeza hatari ambazo wanawake na wasichana wanakabiliana nazo kila siku. Wakati huo huo, kupungua kwa ufadhili kunadhoofisha vuguvugu la utetezi wa haki za ufeministi na huduma muhimu ambazo zinasaidia waathirika katika kutetea usalama na mabadiliko ya kudumu. Zana hizo ni kama zifuatazo;

1. Kampeni katika Mitandao ya Kijamii

Jiunge na kampeni za kikanda! Tutatumia majukwaa yetu ya mitandao ya kijamii ili kupaza sauti zetu. (Facebook, Instagram, Bluesky), jiunganishe, jumuika, na tuendeleze maono yetu ya pamoja ya mustakabali wa kifeministi. Wakati wa kampeni, pia tutashirikisha vibonzo vya Kampeni ya Mitandao ya Kijamii ambavyo wewe pamoja na shirika lako mnaweza kushirikisha kwenye mitandao yenu. Kumbuka kutumia hashtags zilizo hapa chini ili kujiunga: @preventgbvnet.bsky.social, preventgbvnet (Instagram), GBV Prevention Network (Facebook) na kukuza ujumbe wa kampeni.

- Tumia alama za reli hizi:
- #16DaysOfActivism
- #FeministFutures
- #EndOnlineViolence





Unachoweza Kufanya Mtandaoni: Shirikisha mshikamano wako kwa kutuma ujumbe mtandaoni ambao utaonyesha jinsi kikundi au jamii yako inavyosaidia kutokomeza ukatili. Shirikisha ujumbe wenye matumaini, kutia nguvu, na unao unga mkono. Wito kwa kila mtu aheshimu na kulinda utu na faragha ya wengine. Usishirikishe au kusambaza picha au maudhui ya faragha bila idhini, mara tu ukiweka mtandaoni, yanaweza kuenea bila kudhibitiwa na inaweza kuchangia ukatili dhidi ya wanawake. Tuvunje minyororo na kuwa sehemu ya utamaduni wa kuheshima, usalama na uwajibikaji.

Jadili Kuhusu Kupunguzwa kwa Ufadhili: Huku kukiwa na ongezeko la kupunguzwa kwa ufadhili, linalosababisha rasilimali kupungua sambamba na ongezeko la upinzani dhidi ya kazi ya haki za kijinsia, ambao unatishia maendeleo yaliyopatikana kwa juhudi kubwa, kuzima sauti za walio mstari wa mbele katika mapambano, na kudhoofisha mifumo muhimu ya usaidizi ambayo jamii huitegemea. *Chapisha michoro rahisi inayoonyesha kinachoweza kutokea wakati huduma zinapokosa ufadhili. Shirikisha nukuu au hadithi za watu walioathiriwa na ufadhili wa kiwango kidogo.*

Tunakabiliana na changamoto za kipindi hiki kwa kudumu katika misingi ya mshikamano na kujijali kwa pamoja, na kupata nguvu kutoka kwenye mtandao wetu, kurekebisha mikakati yetu kwa ubunifu na ustahimilivu, na kuendelea kupaza sauti na nguvu za wale walioathiriwa zaidi na Ukatili Dhidi ya Wanawake Tafakari juu ya njia mbadala za kufadhili vuguvugu letu.

Kutoka kwenye Changamoto: Wakati kukiwa na changamoto, tunaona fursa zinazojitokeza kwa kasi inayoongezeka juu ya harakati za kutetea haki za kifeministi, kujumuika kwa njia ya kidijitali, na uanaharakati unaoongozwa na vijana. Kwa kukuza nafasi hizi, na kuwekeza kwenye uongozi wa pamoja, na kurejesha masimulizi, tunaweza kujenga siku zijazo zenye msingi wa haki, utunzaji, na mabadiliko ya kudumu ya kijamii. Kuongezeka kwa utetezi kunatengeneza muungano wenye nafasi kwa ajili ya maazimio yalio jumuishi zaidi, yanayoendeshwa na jamii. Kwa kusikiliza kwa kina sauti mbalimbali na kujenga mshikamano wa harakati mbalimbali, tunaweza kuimarisha matokeo ya pamoja na kuhakikisha kuwa hakuna anayeachwa nyuma.

Fanya kazi na Wenye Ushawishi waliopo Nchini: Waombe viongozi wa jamii katika eneo lako, wanaharakati vijana, au washawishi wa mitandao ya kijamii kushirikisha ujumbe wa kampeni. Shirikisha vidokezo kuhusu usalama mtandaoni kwa wanawake na wasichana. Tuma maelezo ya jinsi ya kufanya iwapo mtu atanyanyaswa mtandaoni. Andaa au tangaza kipindi kifupi cha mtandaoni juu ya kujilinda kidijitali.

2. Tumia Redio na Runinga kufikia watu wengi zaidi

Tumia redio na Runinga kupaza sauti kuhusu Siku 16 za Uanaharakati. Shirikisha simulizi za walionusurika (kwa ridhaa), waangazie viongozi na wataalam wa eneo hilo kuhusu masuala kama vile ukatili wa mtandaoni na upungufu wa ufadhili, husisha vikundi vya kijamii vinavyounga mkono haki za wanawake na wasichana, na kuhamasisha matukio ya kampeni ili kuhamasisha kuchukua hatua na mshikamano

Sampuli ya Ujumbe wa Redio/ Runinga (Matangazo kwa Umma-PSAs):





- *“Ukatili dhidi ya wanawake sio suala la mtu kibinafsi; ni suala la jamii. Wakati huduma za usaidizi zinapokosa ufadhili, waathirika hulipa gharama. Ni lazima kutafuta ufadhili kwaajili ya siku zijazo.”*
- *“Wahanga wanahitaji maeneo salama na usaidizia kutoka kwenye nyumba salama hadi usalama wa kidijitali, lazima tuchukue hatua sasa.”*
- *“Kila inapotokea migogoro, wanawake hujitokeza. Jiunge nasi kuunda dunia ambayo utunzaji, usalama, na haki ni kwa kila mtu.*
- *“Kutokomezwa ukatili wa kijinsia si kazi ya mtu mmoja, ni kazi ya wote. Familia, viongozi, jamii, kwa pamoja tunaweza kuunda mustakabali wa utu, usalama na usawa.*

3. Shughuli za Kijamii na Vikundi

Mnachoweza Kufanya kwa Pamoja: Kwa pamoja, mnaweza kuandaa matukio madhubuti yakijamii wakati wa Siku 16 za Uanaharakati. Anzisha mazungumzo kuhusu usalama mtandaoni au njia za kuwasaidia walionusurika. Andaa tukio la kuomba ufadhili wa ndani ili kuimarisha kikundi chako au kuunga mkono shirika la kutetea haki za wanawake. Chora picha za ukutani au sanaa kwa ajili ya kutoa ujumbe wa matumaini na mshikamano. Au andaa kusanyiko kwaajili ya tukio la kushirikishana simulizi na walionusurika na wazee ili kupata hekima, uponyaji, na kuunganishwa.

4. Fanya kazi na Vyombo vya Habari vya Ndani ya Nchi

Vidokezo vya Vyombo vya Habari: Kushirikiana na wanahabari na vyombo vya habari kunaweza kusaidia kueneza ujumbe wako kwa upana wakati wa Siku 16 za Uanaharakati. Tafuta waandishi wa magazeti na vituo vya redio vya karibu ili kuangazia matukio na shughuli zako. Andika makala fupi au maoni kuhusu masuala kama vile matumizi mabaya ya mtandaoni au changamoto za ufadhili. Shirikisha hadithi za matukio yanayotokea nchini yanayohusu ustahimilivu na mabadiliko ya kina. Sherehekea ushindi mdogo ili kuhamasisha na kuunganisha jamii yako.

Taarifa Kwa Vyombo Vya Habari Itakayotolewa Kwa Haraka

Siku 16 za Uanaharakati za mwaka 2025: Wito wa kufikiria upya mustakabali wa Kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake. Mwaka huu, Mtandao wa Kuzuia UWAKI unatoa wito kwa wanachama wake na vuguvugu la kifeministi katika kanda zote katika mapambano, mshikamano, matumaini, na fikra zenye ujasiri. Huku kipindi cha mwaka wa 2025 cha Siku 16 za Uanaharakati Dhidi ya Ukatili wa Kijinsia kikianza, tunatoa wito wa kutafakari mustakabali wa ufeministi ambapo tunaishi katika haki, na uponyaji unapewa kipaumbele, na jamii ni msingi wetu.





Kauli mbiu ya mwaka wa 2025, **“Fikiria Upya Mustakabali wa Kifeministi: Kuimarisha Mshikamano, kustawi baada ya Migogoro,”** inatuhimiza kukabiliana na hali halisi mbaya na kudai mabadiliko. Duniani kote, juhudi za kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na wasichana zinakabiliwa na kupungua kwa nafasi ya raia, kupungua sana kwa ufadhili, na vitisho vya kidijitali vinavyoongezeka. Unyanyasaji, kutoa taarifa ya kugushi kwa njia ya kutumia akili mnemba, kumchimba mtu, na ufuatiliaji sio jambo la kawaida; hubeba matokeo halisi kwa usalama, afya ya akili, na ushiriki katika masuala ya kijamii. Wakati huo huo, programu muhimu za kuandaa sehemu salama zinazowasaidia walionusurika zinavunjwa, na kuacha walio hatarini zaidi kubeba gharama ya kutochukua hatua.

Ukatili Dhidi ya Wanawake unaongezeka kwa kiwango cha hali ya juu duniani kote ikionyesha kuwa mwanamke 1 kati ya 3 alifanyiwa ukatili wa kimwili na kingono katika maisha yake yote. Katika Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara, asilimia 33% ya wanawake wamefanyiwa ukatili wa kimwili au kingono na wapenzi wao wa karibu, ikilinganishwa na asilimia 20% ya wanawake duniani kote. Mmoja kati ya watano (20%) katika eneo la Pembe ya Mashariki na Kusini mwa Afrika alikabiliwa na ukatili uliotendeka mwaka uliopita, ikilinganishwa na asilimia 13% duniani kote (UN Women 2022, Briefs on To End on Ending Violence Against Women).

Kutokomeza UWAKI kunahitaji dhamira ya dhati na endelevu kutoka kila sehemu ya jamii; serikali, taasisi, na watu binafsi pia. Inatakiwa kuwawajibishe wahalifu, kubadilisha kanuni mbaya, na kuwekeza katika mbinu za kuzuia na kulinda zinazoleta matokeo. Hatuwezi kuvumilia kuridhika. Gharama ni kubwa mno, na athari yake ni mbaya sana.

Kampeni hii inatoa wito wa kuchukua hatua, kwa ujasiri wa pamoja, ustahimilivu, na azimio la pamoja. Inatukumbusha kuwa vuguvugu la ufeministi tunalostahili la siku zijazo tunalo lijenga linahitaji maono, rasilimali na umoja. Kampeni hii ya Siku 16 za Uanaharakati ni harakati ya mabadiliko makubwa. Ina tukumbusha kwamba Ukatili sio kuwa hauepukiki kamwe, na wahanga wanastahili kuungwa mkono, si kunyamazishwa. Ni wito wa kujumuika kwa pamoja, katika mshikamano, kwa haraka, huruma, na ustahimilivu.

Hebu sote tuchukue hatua katika kujenga mustakabali ambao wanawake, wasichana, na watu wa jinsia tofauti wanaweza kuishi bila ukatili na uoga. Tunatarajia kusikia hadithi na uzoefu wako!

